# KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

**Tumia viteuzi mwafaka kujazia nafasi 1 - 15.**

Visa vya ujambazi vimewahangaisha ___1___ wa nchi yetu.Kuna aina mbalimbali za wizi. ___2___ hawa hutofuatana kulingana na njia wanazozitumia kuiba. Kuna ___3___ambao hutoa pesa mfukoni na ___4___ambao hutumia silaha.Wengine huwangoja watu njiani na kuwapiga ___5___ kwa kutumia mikono yao. Wakisha ___6___ mtu humnyanganya kila kitu na kumwaacha hali tabaani.

Umoja wa wananchi ndiyo ngao yao. Endapo mtu amevamiwa anastahili kupiga ___7___ na majirani ___8___ watoka chapuchapu ili ___9___ .Tukifanya hivyo watakuwa na nafasi kubwa ya kufanitaiwa. Ijulikane wazi kuwa umoja ni nguvu we utengano ni udhaifu vile vile tuelewe kwamba kidole kimoja hakivunji ___10___

Serikali pia ina ___11___ la kuwalinda wananchi wake. Askari wanapaswa kushika ___12___ usiku ili kuwatia ___13___ watu wowote wenye nia ya kuvunja sheria. Washukiwa wote wapelekiwe ___14___ ili hakimu atoe hukumu. Mshtakiwa anaweza ___15___ au kukanusha mashtaka lakini hatimaye uamuzi wa haki hufikiwa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | wananji | wanainchi | wananchi | wanaichi |
| 2. | mapwaguzi | madalali | hamali | wahandisi |
| 3. | wachochezi | wachopuzi | mapwangu | mapwaguzi |
| 4. | magaidi | majangili | wezi | majambazi |
| 5. | chanja | kapa | kabari | kupe |
| 6. | kwida | nyonga | chinja | kaba |
| 7. | usiahi | kamsa | kabsa | kelele |
| 8. | zao | yake | wake | zake |
| 9. | kumtesa | kumkemea | kumwauni | kumshauri |
| 10. | chawa | kupe | bata | nyoka |
| 11. | wajibu | jukumu | majukumu | mujibu |
| 12. | kwata | sachi | kelele | doria |
| 13. | jelani | mbaroni | mahakamani | kortini |
| 14. | jela | kortini | kortini | gerezani |
| 15. | kukiri | kukataa | kukanusha | kutatanisha |

**Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Muda wa siku kati ya udhuhuri na magharabi ni
A. alfajiri B. jioni
C. alasiri D. asubuhi

17. Andika tarakimu hii kwa maneno **30, 002**
A. elfu thelathini na mbili.
B. thelathini na mbili elfu.
C. thelathini elfu na mbili.
D. elfu thelathini na mbili na mbili.

18. Ni sentensi ipi iliyoakifishwa sahihi.
A. nataka kuzuru visiwa vya ngazija.
B. Lo! mbona hukuja jana.
C. Mzazi wangu alingamua ukweli.
D. Tutakula nyama, wali na matunda.

19. Chagua tashibihi sahihi kujazia nafasi kwenye sentensi.
Msichana huyu ni msiri kama ______
A. mchana B. kaburi
C. mchawi D. giza

20. Tumia kiulizi mwafaka
Unataka kikapu ______
A. gani B. kigani
C. yupi D. ngani

21. Kanusha sentensi.
Kusoma kuna faida.
A. kutosoma hakuna faida.
B. kusoma hakuna faida.
C. kusoma kuna faida.
D. kutosoma kuna faida.

22. Ndugu wa kike wa baba utamwitaje?
A. Ami B. Bibi
C. Shangazi D. Halati

23. Miradi mingine iliharibika
Neno "mingine" ni
A. kiwaki B. kivumishi
C. kitenzi D. kielezi

24. Kamilisha methali ifuatayo
Dalili ya mvua ni
A. radi B. rasharasha
C. mawingu D. upinde

25. Tegua kitendawili
Inzi hatui juu yangu.
A. neno B. jua
C. moto D. nanasi

26. Teua sentensi iliyotumia **ki** ya masharti
A. Kiatu chake ni kikubwa.
B. Kijibwa kile ni cha kike.
C. Kipi ndicho kilivunjia?
D. Nikienda mapema nitapongezwa.

27. Wewe ______ uliyemwangusha mtoto.
A. ndiye B. ndio
C. ndiwe D. ndiyo

28. Andika sentensi ifuatayo kwa wingi.
Karatasi yoyote nyingine inanifaa.
A. Karatasi zozote zingine zinanifaa.
B. Makaratasi yoyote mengine yanatufaa.
C. Karatasi zozote nyingine zinanifaa.
D. Karatasi zozote nyingine zinatufaa.

29. Bizari, mdalasini na tangawizi kwa jumla ni
A. mapochopocho
B. michuzi
C. vyakula
D. viungo vya mapishi

30. Teua kielezi kwenye sentensi
Mwanafunzi mtundu atahadhibiwa vikali.
A. vikali B. mtundu
C. adhibiwa D. mwanafunzi

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.**

Kashere aliamka na bila kupoteza wakati alielekea bafuni kuoga. Alikuta kuwa maji hayakuwa bafuni kama ilivyokuwa desturi. Alikumbuka kuwa shangazi yake ambaye alikuwa amejitwika jukumu la kumpelekea maji bafuni alikuwa amesafiri kumtembelea mama yake. Alijawa na ghaidhi kwa sababu alijua kuwa angechelewa na walimu wake hawakuwahurumia watepetevu. Aliwazia kuoga kwa maji baridi shadidi lakini wazo hili akalitupilia mbali kwa vile baridi ilikuwa ikizizima. Alienda jikoni na kuwasha moto chapuchapu.Kuni zilikuwa zimekauka vizuri muda si muda maji yalichemka. Alitia kwenye karai na kuyazimua. Aliyabeba taratibu hadi hamamuni. Alioga haraka haraka. Mawazo yalikuwa yakimzunguka kichwani kama pia . Mwalimu wa zamu hakuwa mtu wa kusikiliza hadithi za uongo. Kashere hakutaka kudhibewa. Aliwazia jambo lolote la mumdanganya

lakini akashindwa kwa sababu hakuwa bora katika kusema uongo. Alishindwa hata kunywa kiamshakinywa. Alivaa harakaharaka na kutoka mbio kama swara anayefukuzwa na simba Hivyoo!

Mbio zake hazikumsaidia kitu. Alikuwa amechelewa. Aliwakuta wanafunzi wengine kwenye gwarinde. Alipojitokeza tu wanafuzi wote waliangua vicheko vya radi. Hakuelewa kwa nini waheheka hivyo. Alidhani kuwa alihekwa kuhusu adhabu ambayo alikuwa apewe. La kushangaza ni kuwa alikuwa amevaa kaptura ndani nje, shati halikuwa sare ya shule na viatu vilikuwa vya rangi tofauti kimoja chekundu kingine cheusi. Alishtuka sana lakini alijikakamua na kumsimulia mwalimu kisa chote kinaganaga. Mwalimu alitabasamu na kumwambia Kashere kuwa alimsamehe kwa sababu alisema ukweli nao ukweli humweka mtu huru.

Wanafunzi walifunzwa kuhusu umuhimu wa kijitegemea badala ya kungoja kufanyiwa kila kitu. Walifahadharishwa kuhusu kuwacheka na kuwakebehi wenye matatizo kwani hakuna anayependa kuwa na ila yoyote

Kashere aliruhusiwa kurudi nyumbani ili avae sare rasmi kwa njia inayofaa.

31. Chagua sentensi sahihi
   A. Kashere alichelewa kwa kuwa alichelewa kuamka.
   B. Kashere aliishi na wazazi wake.
   C. Kashere aliamka mapema sana .
   D. Shangaziye ndiye aliyechelewa kuamwamcha.

32. Ni mazoezi yapi aliyokuwa nayo shangaziye Kashere?
   A. Alizoea kumpelekea Kashere maji bafuni.
   B. Kumwosha Kashere.
   C. Kumtesa Kashere.
   D. Kumwadhibu kila alipokosea.

33. Kashere alikuwa mwanafunzi wa aina gani?
   A. Aliyekuwa na mazoea ya kuchelewa.
   B. Alichelezea kuvunja sheria za shule kwa sababu angeadhibiwa.
   C. Alikuwa haogopi adhabu ya mwalimu.
   D. Alikuwa mzembe shuleni.

34. Walimu katika shule iliyotajwa
   A. walikuwa hodari katika kufunza
   B. walikuwa hawapendi uvivu.
   C. waliwapa msamaha wanafunzi wavivu.
   D. waliwasili shuleni wakiwa wamechelewa

35. Kwa nini Kashere hakuoga kwa maji baridi?
   A. Maji yalikuwa yamepashwa moto.
   B. Shangazi yake alimuzuia asifanye hivyo.
   C. Aliogopa kuugua homa.
   D. Kulikuwa na baridi sana.

36. Hatimaye alioga kwa maji
   A. fufutende
   B. moto
   C. moto baridi
   D. baridi

37. Habari hii inatueleza kuwa Kashere alithamini
   A. uongo
   B. ubadhirifu
   C. ukweli
   D. utepetezi

38. Kwa nini wanafunzi waliangua kicheko Kashere alipowasili?
   A. Kwa sababu walikuwa kwenye gwaride.
   B. Wanafunzi walihumia kwa kichapo ambacho angekipokea.
   C. Walikuwa na tabia ya kucheka kila mwanafunzi alipochelewa.
   D. Licha ya kuchelewa Kashere alikuwa amevaa nguo nje.

39. Ni kitendo kipi cha maadili ambacho mwalimu wa zamu alifanya?
   A. Alimwambia kashere arudi nyumbani.
   B. Badala ya kumwadhibu aliwafunza wanafuzi kuhusu umuhimu wa kujitegemea
   C. Aliwaruhusu wanafuzi wamcheke Kashere ili ajifunze.
   D. Alimsamehe na kumwambia aende darasani.

40. Teua kichwa mwafaka cha habari hii
   A. Haraka haraka haina baraka.
   B. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe
   C. Ngoja ngoja huumiza matumbo.
   D. Kidole kimoja hakivunji chawa.

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41- 50.**

Ulimwengu wetu unazidi kila uchao. Mabadiliko haya hasa hutotaka na teknolojia ngeni ambayo imezidi kuborosha na kuzirahisisha shughuli za binadamu.

Katika mstari wa mbele ni uvumbuzi wa simu za mkononi. Simu hizi ambazo pia huitwa simu tamba au rununu zimerahisisha hali ya mawasiliano kabisa. Kwa kutumia simu hizi unaweza kuwasiliana na walio mbali kabisa bila kutumia nyaya. Unaweza pia kuwasiliana na aliye mbali kwa kutumia ujumbe mfupi kwa gharama ndogo sana. Rununu pia hutumika kama kamera na redio.

Aidha kuna chombo cha tarakilishi. Tarakilishi hutumika ofisini na hata nyumbani. Chombo hiki hutumika katika kupiga chapa, kufanya hesabu na kuhifadhi maandishi. Maandishi haya huafandhiwa katika disketi tepetevu.

Waruti nao pia umerahisisha mawasiliano kupindukia kwa kutumia mtandao wavuli , unaweza kuwasiliana na yeyote aliye popote duniani na wakati wowote. Kwa hivyo, sio watu wengi wanaoendelea kutumia masanduku ya posta.

Runinga nayo ni chombo kinachotoa sauti pamoja na kuonyesha picha zenyewe. Runinga hupendwa sana kwa sababu mawasiliano yake ni moja kwa moja na matangazo yake huwafikia watu wengi wakati mmoja. Runinga pia hutumika kuonyesha vipindi vya kuelimisha na kuburudisha mno.

41. Kipi si chombo kinachotokana na teknolojia ya sasa?
 A. Runinga  B. Saa
 C. Rununu  D. Tarakilishi

42. Ipi si kazi ya simu ya mkono kati ya zifuatazo?
 A Kupiga picha.
 B. Kutuma ujumbe mfupi.
 C. Kupiga chapa.
 D. Kuwasiliana na aliye mbali.

43. Maandishi huifadhiwa katika
 A. disketi tepetevu  B. redio
 C. mtandao  D. runinga

44. Neno aidha limepigiwa mstari, lina maana gani?
 A. Sivyo  B. Ingawa
 C. Tena  D. Ama

45. Kulingana na habari
 A. watu wengi hutumia masanduku ya posta.
 B. sio watu wengi wanaotumia masanduku ya posta.
 C. Mtandao waruti ni ghali mno.
 D. Mtandao waruti hupatikana kila mahali.

46. Ni chombo kipi kinachotoa sauti na kuonyessha picha wakati mmoja
 A. sanduku la posta
 B. redio
 C runinga
 D eropleni

47. Ukitaka kuwapasha watu wengi ujumbe wakati mmoja utatumia
 A. mtandao waruti.
 B. runinga
 C. rununu
 D. tarakilishi

48. Neno jingine lenye maana sawa na tarakilishi ni
 A. Kamere  B. Komputa
 C. Compyuta  D. Kompyuta

49. Vyombo vyote vifuatavyo hutumika katika mawasiliano ila
 A. simu tamba  B. runinga
 C. mtandao wavuti  D. kamera

50. Taarifa hii yahusu
 A. Ulimwengu wetu wa kisasa.
 B. Teknologia ya kisasa.
 C. Elimu ya kisasa.
 D. Mawasiliano.